

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية الجاليات بالزلفي

مشروع تعلم الإسلام - أحكام الطهارة - سواحيلي

Samo la 4

الدرس الرابع

UDHU.

Haikubaliwi swala ya mtu bila ya kuwa na udhu.

Hadithi iliyopokelewa na Abi Huraira (R.A) Mtume (saw) anasema ("Hakika ya mwenyezi mungu haikubali swala ya mmoja wenu pindi anapotokwa na udhu mpaka atawadhe") (Ameipokea Bukhar na Muslim :6954, 225).

فَعَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - قَالَ: «إِنَّ اللَّهَ لَا يَكْبُلُ صَلَةً أَحَدَكُمْ إِذَا أَحَدَثَ حَتَّى يَتَوَضَّأْ» [متفق عليه: 6954].

Hapana budi anapo tawadha afuate taratibu na kuutiliza kiungo kimoja baada ya kingine wakati wa kutawadha.

Udhu una fadhila kubwa sana inatakikana mtu apate hisia ya kuwa anafanya kitu chenyethamani kubwa kama ilivyo kuja kwenye hadithi ya Swahaba mkubwa wa Mtume (saw) Othman bin Affaan (R.A) anasema, amesema bwana Mtume (saw): (Mwenye kutawadha akaufanya uzuri udhu wake, yatatoka madhambi yake kutoka mwilini mpaka chini ya kucha zake) (Ameipokea Imam Muslim: 245).

عَنْ عَمَّارِ بْنِ عَفَانَ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ -: «مَنْ تَوَضَّأَ فَأَحْسَنَ الْوَضْوَءَ ، خَرَجَتْ خَطَايَاهُ مِنْ جَسَدِهِ ، حَتَّى تَخْرُجَ مِنْ أَطْفَارِهِ» [رواه مسلم: 225]. وَعَنْهُ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ -: «مَنْ أَتَمَ الْوَضْوَءَ كَمَا أَمَرَ اللَّهُ تَعَالَى ، فَالصَّلَوَاتُ الْمُكْتَوَبَاتُ كُفَّارٌ لَمْ يَبْيَنُوهُنَّ» [رواه مسلم: 231].

Na imepokelewa kutoka kwa Othman (R.A) ya kuwa Mtume (saw) anasema : (Mwenye kutimiza udhu kama alivyo amrisha na mwenyezi mungu, basi swala tano za faradhi ni kafara la kufutiwa madhambi kati ya kila swala) (Ameipokea Imam Muslim:231).

NAMNA YA KUTAWADHA.

1. Atanuia kutawadha moyoni mwake bila ya lutamka kwa ulimi, na nia ni kuazimia jambo au kitu moyoni, kisha atasema Bismillah.
2. Kisha ataosha viganja vyake mara tatu.
3. Kisha atasukutuwa na kupandisha maji puani mara tatu.
4. Kisha ataosha uso wake mara tatu, kuanzia sikio mpaka sikio upana, na kuanzia sehemu iliyoota nywele kichwani mpaka chini ya kidevu urefu.
5. Kisha ataosha mikono yake mara tatu, kuanzia kwenye vidole mpaka kwenye kongo mbili, kwa kuanzia mkono wa kulia kisha mkono wa kushoto.
6. Kisha atapangusa kichwa chake mara moja, ailoweshe mikono kisha aipitishe kuanzia mwanzo wa kichwa mpaka nyuma ya kichwa kisha airudishe mpaka mwanzo alipoanza.
7. Kisha apanguse masikio yake mawili, aingize vidole vyake vya shahada kwenye tundu za masikio, na utapangusa juu ya masikio yake mawili kwa vidole gumba.
8. Kisha ataosha miguu yake miwili mara tatu, kuanzia kwenye vidole pamoja na nguyu mbili (vifupa viwili vilivyoko mguuni) akianzia mguu wa kulia kisha mguu wa kushoto.
9. Kisha inapendeza akiwa ataomba dua hii iliyokuja baada ya kumaliza kutawadha:

أشهد أن لا إله إلا الله ، وأنَّ محمداً عبدُه ورسولُه

(Nashudia ya kwamba hapana mola anaestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa mwenyezi mungu pekee, na ninashudia ya kwamba hakika ya Muhammad ni mja wake na mtume wake.)

فَعَنْ عُمَرَ بْنِ الْخَطَّابِ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ - قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ -: «مَا مِنْكُمْ مَنْ أَحَدَ يَتَوَضَّأْ فَيُسْبِحُ الْوَضْوَءَ ثُمَّ يَقُولُ: أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ، وَأَنَّ

[رواه مسلم: 234].

Hadithi aliyopokea swahaba Umar bin Khatwab (R.A) anasema: Amesema bwana Mtume (saw) kuwa: (Hayupo yejote mionganii mwenu akatawadha akaufanya vizuri udhu wake kisha akasema: Nashuhudia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa mwenyezi mungu, na ninashudia ya kuwa Muhammad ni mja wake na mtume wake, isipokuwa atafunguliwa siku ya kiyama milango minane ya peponi, aingie mlango wowote autakao) (Ameipokea Imam Muslim: 234).